**Learning by Ear**

**"Everyone's Different – Respect for Minorities"**

**Episode 03**

**Title: Young Zimbabweans Fighting the Stigma of HIV**

**Author: Columbus Mavhunga**

**Editor: Katrin Ogunsade, Friederike Müller**

**Proofreading: Charlotte Collins**

**Characters (O-Töne, Clips) / Narrators**

| | | | |
|---|---|---|---|
| ***Narrator*** | male | about 35 | english |
| ***Brian (clip)*** | male | 23 | english |
| ***Alex (clip)*** | male | 21 | english |
| ***Chengetai Dziwa*** | male | unimportant | english |
| ***Dr Nyika Mahachi*** | male | unimportant | english |
| ***Johannes*** | male | 29 | english/shona |
| ***Rue*** Pronunciation: Roo = "ru" in "Rude" | female | 22 | english |

**Pronunciation:**

Brian (Brian)

Alex (Alex)

Nyika Mahachi (Nyi (as in "new" on "nyi," while "i" sounds as in "e")- ka [Mah-har-chi])

Johannes (as written)

Rue (Roo, as in "ru" in "Rude")

Chengetai Dziwa (Che-nge-ta-yi [Dzi (-ds) -wa])

**Intro:**

Hujambo na karibu kwenye kipindi chetu cha -Noa Bongo Jenga Maisha Yako kinachoitwa, "**Kila mtu ni tofauti-Kuzingatia maslahi ya jamii za walio wachache**". Kwenye sehemu hii ya tatu tutakutana na vijana wa Kiafrika ambao watatuelezea kuhusu unyanyapaa unaowakumba waathiriwa wa UKIMWI barani Afrika. Vijana hao watatueleza jinsi wanavyokabiliaana na jambo hilo. Ungana nasi tunapoitembelea nchi ya Zimbabwe, ambayo ina kiwango cha juu zaidi cha maambukizi ya UKIMWI miongoni mwa nchi za Afrika, Kusini mwa jangwa la Sahara.

1. **SFX HIV positive youths talking**

2. **Narrator**

Vijana hawa wanaishi na virusi vya Ukimwi. Wao hukutana kila Jumamosi alasiri katikati ya mji mkuu wa Zimbabwe, Harare kuzungumzia tajiriba zao. Mmoja wao tutampa jina la Brian mwenye umri wa miaka 23. Anasema kwamba alizaliwa akiwa na virusi vya Ukimwi. Wazazi wake wawili walifariki kutokana na Ukimwi. Anasema alitatizika sana kwa sababu ya unyanyapaa punde baada ya kujigundua kuwa na virusi vya Ukimwi alipokuwa na umri wa miaka 10.

***KW begin***

3. **Soundbite Brian (English)**

*"Nipotambua kwamba nilikuwa na virusi vya Ukimwi, niliteseka sana kwa kujinyanyapaa mwenyewe binafsi. Ingawa pia kulikuwa na unyanyapaa kutoka kwa watu wengine. Hata shuleni. Kauli zilizotolewa. Hata michezo yao hainipendezi. Hakunitukana hata kidogo. Lakini mambo waliokuwa wakisema kunihusu: '**mbona midomo yako ni miekundu, na mbona***

***maradhi hayakutoki**? **Mara juma moja unakuwa shuleni, juma jingene unakuwa nyumbani**…'*

***KW end***

**4. Narrator**

Leo, Brian amevumbua njia ya kukabiliana na uyanyapaa na ubaguzi: Hajishughulishi tena na mambo hayo.

**5. Soudbite Brian (English)**

*"Kwanza niliikiri hali yangu. Haitabadilika. Tiba ya kwanza ni huko kukubali hali yangu….Pili ninatumia dawa jinsi nilivyoagizwa na madaktari. Jambo muhimu zaidi kwa wagonjwa wa Ukimwi ni kutumia dawa jinsi wanavyoagizwa."*

**6. Narrator**

Brian sasa anazungumza kama daktari au mshauri. Asemavyo ni kweli: ni muhimu kuzingatia matibabu. Mtu anaweza kuwa na virusi vinavyosababisha Ukimwi kwa muda mrefu bila huo Ukimwi kudhihiri. Matibabu husaidia kudhibiti virusi hivyo na kupunguza kasi ya maambukizi. Hapo mjini kuna ukumbi unaoitwa "Zvandiri House," ambao ni makao ya Shirika la Misaada la Afric Aid.

**7. SFX: HIV discussion/arrival at the offices**

**8. Narrator**

Ni shirika linaloshughulikia vijana wanaoishi na virusi vya Ukimwi. Zvandiri ni tamko la lugha ya Kishona lenye maana " Hivi nilivyo." Vijana hao waishio na virusi vya Ukimwi waliibua tamko hilo kwa nia ya

kuwaambia walimwengu, "**Mtukubali jinsi tulivyo**." Alex alitambua kuwa ana virusi vya Ukimwi mwaka 2007 alipokuwa na umri wa miaka (16) kumi na sita. Sasa hivi anafanya kazi ya mshauri wa kujitolea. Alex anasema angetaka vijana wote wa Zimbawe wapimwe damu ili wajue hali zao za afya. Anapoulizwa kwa nini anataka hivyo, anatabasamu, kisha anasema:

**_9._ Soundbite Alex**

*"Sasa hivi nimeridhika kujua hali yangu. Kila mara mtu huishia kuwa na maswali mengi: Kwa nini mimi huugua kila mara, Kwa nini sihudhurii masomo. Lakini pale unapojua sababu, unapata fursa kushughulikia ndoto zako ipasavyo. Ninajivunia kuwa jinsi nilivyo. Nimeshazoea… wala sihuzuniki."*

**10. Narrator**

Alex anataka kuwa muuguzi siku za usoni ili awasaidie vijana wengi wa Zimbabwe kupambana na Ukimwi. Lakini si hilo tu analotamani kutimiza siku za usoni.

**_11._ Soundbite Alex**

*"Ninataka kuoa na kupata watoto. Pengine miaka mitano …*

***KW begin***

*Sasa hivi, nina mchumba. Ninampenda sana. Lakini tuna matatizo kama walivyo binadamu wengine. Tunajikaza."*

***KW end***

**12. Narrator**

Alex na Brian ni miongoni mwa vijana ambao wamefanikiwa kuishi bila kushughulishwa na unyanyapaa kwa kuwa wana virusi vya Ukimwi. Hata hivyo kuna baadhji ya vijana waliokumbana na changamoto nyingi.

13. **Soundbite Rue**

*"Nilipopimwa, mama yangu hakunifahamisha. Alinieleza habari hiyo baada ya miaka mitano. Hakunitendea haki. Pengine alikuwa na sababu zake maalumu, baadaye nilibaguliwa sana hata na jamaa zangu.*

14. **Narrator :**

Tutamuita msichana huyu mwenye umri wa miaka ishirini na miwili, (20) Rue. Kwa sasa hivi msichana huyu ni mshauri wa kujitolea wa Shirika la Afric Aid kama vile Alex. Anasema nduguye wa kiume hakumruhusu kujichagulia masomo aliyotaka kusoma shuleni. Pindi alipogundua kuwa alikuwa na virusi vya Ukimwi, ndugu yake akaanza kumuamlia mambo, kumchagulia marafiki na hata kumweleza nyakati alizopaswa kulala.

***KW begin***

15. **Soundbite Rue**

*Hizi ndizo baadhi ya changamoto ambazo pia ziliathiri uamuzi wangu wa kazi nilizotaka kufanya-kufikia umri fulani niliamua kujiunga na masomo ya uuguzi. Hata hivyo, kujiunga na uuguzi si jambo rahisi kwa kuwa wanazingatia pia hali zetu za kiafya. Kwa hivyo kuna changamoto nyingi sana."*

***KW end***

16. **Narrator**

Hivi leo, ndugu yake alitenda aliyoyatenda kwa kutojua.

**17. Soundbite Rue:**

*"Sasa hivi, sijihisi kwamba ninabaguliwa. Pengine ndugu yangu hakuelewa hali yangu. Alidhani alikuwa akinisaidia kumbe mambo yalikuwa kinyume. Maradhi yangu yalinifanya kuzingatiwa kwa kila hali nyumbani. Ninaelewa fika kilichomfanya ndugu yangu kunitendea alivyonitendea. Ugomvi na vita havikukoma kati yangu na ndugu yangu."*

**18. Narrator:**

Rue angependa kuishi Zimbabwe, nchi yenye utangamano na angependa utangamano huo uwe hata kwenye familia yake. Anasubiri kwa hamu harusi yake mwezi Aprili. Mchumba wake tayari ameshawalipa jamaa za Rue *lobola* – mahari ya kienyeji – ili harusi ifanyike. Mahari hayo nchini Zimbabwe ni fedha taslimu pamoja na kiasi cha ng'ombe kadhaa. Mchumba wake-wa tangu miaka mitatu iliyopita-hana virusi vya Ukimwi. Rue anaeleza hisia za jamaa zake waliposikia kuhusu harusi hiyo inayotarajiwa.

***19.*** **Soundbite Rue**

*"Walistaajabu kwa kuwa watu wengi hawakutarajia. Hata hivyo waliridhia na kuufurahia uamuzi wangu."*

**20. Narrator**

Mchumba wa Rue ni mfanyibiashara mjini Harare na ana umri wa miaka ishirini na tisa (29). Wala haridhii kulizungumia suala hili. Hata hivyo, anakubali kukutana nasi baada ya kazi.

*KW begin*
Tunapowasili nyumbani kwake kiza kimetanda kila mahali: Hakuna nishati ya umeme, ila tu majenereta ya watu wachache ambao wanataka majumba yao yawe na mwangaza.

21. **SFX generator**

22. **Narrator**

Gari letu linafululiza hadi kwenye baa iliyo karibu ambapo mashabiki wa mchezo wa soka wanatizama mechi na pia kusikiliza muziki. Tunaamua kubaki ndani ya gari ili tukipate kisa cha Johannes, mchumba wake Rue.

23. **SFX: Car**

24. **Narrator**

Mwanzoni, Johannes anaonekana kuwa na wasiwasi. Tunafungua madirisha ya gari na kuufaidi muziki unaorindima kutoka kwenye baa iliyo karibu. Hatimaye, Johannes anachangamka. *KW end*

25. **Soundbite Johannes**: (**He mixes English and Shona**)

*"Sitaki kuwa na maisha magumu. Nataka kuchukulia mambo kwa wepesi. Naam! Nilijiuliza hivi nikimuacha Rue: Nitakwenda wapi? Jambo moja tu linalonisumbua mpaka sasa ni jinsi ya kupata mtoto. Lakini tutaoana na tutaishi pamoja maishani mwetu."*

26. **Narrator**

Johannes anasema kwamba hajawaambia wazazi wake kwamba mchumba wake anaishi na virusi vya Ukimwi. Anachelea huenda wasimkubali kuwa mke wake. Kuna madai yasiyokuwa na msingi kwamba watu waishio na virusi vya Ukimwi hawawezi kupata watoto wasiokuwa na virusi. Inawezekana kupata mtoto asiyekuwa na virusi pale mmojawapo wa wahusika hana virusi. Mradi tu wazingatie matibabu ipasavyo. Daktari Nyika Mahachi, anayelifanyia kazi Shirika lisilo la Kiserikali linalokabiliana na unyanyapaa, anaeleza.

**27. Soundbite Mahachi**

*"Kwa sasa hivi, tuna ithibati kwamba matibabu yanayoafiki ni muhimu sana kuzuia mtu aliye na virusi kumuambukiza mwenzake ambaye hana virusi vya Ukimwi.*

*Kwa hivyo, ikiwa mtu ana virusi vya Ukimwi na matibabu yanadhibiti virusi hivyo, hilo linatambulikana kuhesabu chembechembe za damu ama "CD4 count". Hapo basi wahusika wanaweza kupata mtoto.*

***KW begin***

*Sasa hivi, utafiti unaonyesha kwamba ikiwa mtu amekuwa akizingatia matibabu ipasavyo si rahisi kuambukiza mtoto anayezaliwa mradi tu hizo dawa anazotumia hazijawa na madhara kwake."*

***KW end***

**28. Narrator**

Yamkini maelezo ya mtaalamu huyu wa matibabu yakampa matumaini Johannes. Wakati tukisubiri tuone jinsi Johannes atakavyowaeleza wazazi wake kuhusu hali ya afya ya mchumba wake Rue anayeishi na virusi vya Ukimwi. Turejee katika "Zvandiri House". Vijana wanaosihi na VVU wamekuja kwa ushauri nasaha, na huku wengine wakijishughulisha na kazi za mikono.

**29. SFX Metal cutter clips.**

**30. Narrator**

Kijana huyu wa umri wa miaka 20 anatengeneza visahani vya majivu na fremu za picha kwa kutumia makopo ya vinywaji yaliyotumika. Maafisa wa Afric Aid wanasema kwamba anahitaji fedha kwa kuwa tangu wazazi wake walipofariki kwa maradhi ya Ukimwi, yeye ndiye anayewatunza jamaa zake. Kiwango cha maambukizi ya virusi vya Ukimwi nchini Zimbabwe kinaendelea kushuka. Hata hivyo, nchi hiyo ingali na kiwango kikubwa cha vifo vinavyohusiana na Ukimwi miongoni mwa nchi za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara. Takriban watu 2000 hufa kila wiki kutokana na maradhi yanayohusiana na virusi vya Ukimwi. Kwa sababu hii, kuna familia nyingi zinazoongozwa na watoto- na wengi wao wana virusi vya Ukimwi.

**31. SFX: Youths talking**

**32. Narrator:**

Wakuu wa Shirika la Afric Aid wanasema walianzisha harakati za vijana kama vile Alex na Rue kuwatembelea vijana wenzao walio na virusi vya Ukimwi ili kuwahamasisha kukubali hali zao na kuzingatia matibabu. Huyu hapa Chengetai Dziwa, ofisa wa Shirika la Afric Aid.

***33.* Soundbite Dziwa**

*"Miradi yote… inasimamiwa na watoto wenyewe. Rai zao na maoni yao yanazingatiwa. Ili kuhakikisha kwamba vijana wanahusishwa kikamilifu, mabarobaro walio na virusi vya Ukimwi hupawa mafunzo ili wawafunze*

*watoto wengine katika jamii masuala ya matibabu na pia kuwahimiza wasife moyo. Wanakuwa ni kiungo kati ya jamii na kituo cha afya."*

**34. Narrator**

Vijana waishio na virusi vya Ukimwi nchini Zimbabwe wanahitaji mambo mengi ya ziada mbali na matibabu. Ni muhimu pia kuwapa habari na kuwashauri jinsi ya kuishi wakiwa na virusi vya Ukimwi. Mbinu hii itawapa uwezo vijana wa Kiafrika kukabiliana na unyanyapaa unaotokana na virusi vya Ukimwi na pia kuwawezesha kuwahamasisha wenzao ili wasisambaze virusi hivyo. Vijana uliotangamana nao kwenye kipindi hiki ni ithibati tosha kwamba mtu anaweza kuishi akiwa na virusi vya Ukimwi bila tatizo. Vijana hao wamezikiri hali zao ingawa bado hawajakubalika kwa dhati na jamii zao. Wanatumaini kwamba mambo yatabadilika siku za usoni.

**Outro**

Na mpaka hapo, tumefika mwisho wa sehemu ya leo ya kipindi cha **Noa Bongo Jenga Maisha Yako** iliyoshughulikia namna ya kukabiliana na unyanyapaa kutokana na maradhi ya Ukimwi barani Afrika. Kutoka Zimbabwe tulikuwa naye Columbus Mavhunga. Unaonaje hali ya hao vijana walio na virusi vya Ukimwi nchini Zimbabwe? Je! Vijana wengine wa Kiafrika walio na virusi wanafaa kuiga mfano wa vijana hao wa Zimbabwe? Kama kawaida, tungependa kupata maoni yako – tuandikie maoni yako kwenye ukurasa wetu wa Facebook. Ukitaka kusikiliza tena kipindi hiki, au kuwajulisha marafiki zako kukihusu, utapata makala za **Noa Bongo Jenga Maisha yako** katika wavuti www.dw.de/lbe.

Kwa heri kwa sasa – Usikose kututegea siko kwenye sehemu ijayo!